

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



VICE PRESIDENT'S OFFICE  
NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL  
(NEMC)



**TAARIFA KWA UMMA**

Asubuhi ya tarehe 4 Disemba 2023, katika eneo la kijiji cha Makutano (Zero Zero) Wilaya ya Musoma Mkoa Mara, lori lililokuwa limebeba kemikali aina ya Ethanol kiasi cha Madumu 160 yenye ujazo wa lita 250 kila moja lilipata ajali na sehemu kubwa ya kemikali hiyo kumwagika na kuungua. Kemikali hizo ni mali ya DC & Sons Company Limited. Lori pamoja na kemikali hizo viliteketea kwa moto.

Tathmini ya awali inaonyesha kuwa kemikali hizo hazikuwa na madhara makubwa kwa vile sehemu kubwa ya kemikali hizo ziliteketea kwa moto. Hata hivyo, sampuli za maji kwenye eneo hilo zimechukuliwa na timu ya wataalam toka ofisi ya NEMC na Mkemia mkuu wa Serikali kwa uchunguzi zaidi.

Kemikali aina ya ethanol ni kemikali ambayo huwaka kirahisi (Volatile and Flammable) na hutumika katika kutengeneza vileo inapochanganywa katika kiwango kidogo. Vile vile, hutumika katika kutengeneza madawa ya binadamu na vipodozi.

Imetolewa na;

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Samuel G. Mafwenga'.

Mha. Dkt. Samuel G. Mafwenga

**Mkurugenzi Mkuu**